

102/3

KISWAHILI

Karatasi 3

FASIHI

JULAI/AGOSTI – 2011

Saa: 2½

KAMATI YA UIMARISHAJI ELIMU KAUNTI YA BARINGO

Hati ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari (K.C.S.E)

KISWAHILI

Karatasi 3

FASIHI

Saa: 2½

Jibu maswali manne pekee.

*Swali la kwanza ni la **lazima**.*

Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani: Riwaya, Hadithi Fupi, Ushairi na Fasihi Simulizi.

*Usijibu maswali **mawili** kutoka katika **sehemu moja**.*

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

TAMTHILIA**KITHAKA WA MBERIA: *Kifo Kisimani*****1** (Lazima)

“Kuwa katika pindo la chatu na kisha kutojulikana mtu aliko kunaweza kumaanisha ametoroka. Lakini pia kunaweza kumaanisha kwamba umio wa chatu umefanya kazi yake.”

- (a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- (b) Taja na ufafanue sifa za mzungumzaji na mzungumziwa. (alama 10)
- (c) Eleza jazanda iliyotumika katika muktadha huu. (alama 6)

RIWAYA**S. A. MOHAMED: *Utengano****Jibu swali la 2 au la 3***2** ‘Watu wameshachoka kudanganywa na wanafiki kama nyinyi.’

- (a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
- (b) Eleza sifa za msemaji wa maneno haya. (alama 4)
- (c) Wakati wa kisa hiki, msemaji na msemewa wanasababisha aina fulani ya ‘Utengano’. Taja utengano huu na ueleze sababu zake. (alama 4)
- (d) Thibithisha madai kwamba uhuru wa wahusika fulani katika riwaya hii haujatimia. (alama 8)

au**3** Huku ukirejelea wahusika wowote wawili, fafanua mabadiliko kumi yaliyowapata kila moja wao. (alama 20)**HADITHI FUPI****K. W. WAMITILA: *Mayai Waziri wa Maradhi****Jibu swali la 4 au la 5***4.** Eleza matatizo yanayokumba sekta ya elimu ukirejelea hadithi zifuatazo.

- (a) Fumbo la mwana (Sinjiri Mukuba)
- (b) Ndimi za mauti (Timothy M. Agere)
- (c) Mkimbizi (John Habwe) (alama 20)

au

5 “Mnavyojua vizuri na yote hayo si kweli... Hata wengine wenu mmekuwa sungura. Kwani wewe Abdalla ulikuwa humfuatifuati, si hata ulimposa? Nyoo! Basi haifai hata kama hamtampatia kura. ”

- (a) (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
(ii) Eleza ukweli kuhusu mrejelewa katika dondoo. (Alama 2)
(iii) Taja na utoe mfano wa mbinu yoyote ya lugha ambayo imejitokeza katika dondoo. (Alama 2)
(b) Jamii iliyorejelewa katika jamii husika ilisheheni maovu makubwa. Fafanua kauli hii. (Alama 12)

USHAIRI

6 *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Nina jambo muhimu, nyi wakubwa kwa wadogo,
Kuwa tabia alimu, usiubwage gogo,
Mtu kukosa nidhamu, ja mtu akili ndogo,
Tabia njema ni utu.

Walezi nawaambia, wafunze tabia wana,
Ili wanapokua, wenye heshima maana,
Mtu kukosa tabia, ni kama mti bila shina,
Tabia njema ni utu.

Hutuzidisha hisia, kufurahisha roho,
Gumu tuepushia, linalotumiza roho,
Mtu kukosa twabia, nikiumbe bila roho,
Tabia njema ni utu.

Wanafunzi nao pia, shuleni sizushe bala,
Ili masomo kubia, bila mambo ya kifala,
Mtu kukosa twabia, dareva toroli bila,
Tabia njema ni utu.

Mahabani walioa, sio urembo mwingi,
Bali hasa ni tabia, utu mapenzi mengi,
Mtu kukosa tabia, kama nyumba bila msingi,
Tabia njema ni utu.

Shuleni vijijinia, amani dumu kujali,
Sababu kuwa tabia, lizingatiwa aali,

Mtu kukosa tabia, ni kisu bila makali,
Tabia njema ni utu.

Rafiki kukupendea, sio kwa uzuri eti,
Bali ni hasa tabia, ndani yako wima uti,
Mtu kukosa tabia, ni kiumbe bila uti,
Tabia njema ni utu.

Tamati kuachia, kwamba jambo aali,
Mengi ningewambia, lakini metoshekali,
Mtu kukosa tabia, ni kiatu bila soli,
Tabia njema ni utu.

MASWALI

1. Pendekeza kichwa mwafaka la shairi ulilosoma. (alama 1)
2. Shairi hili linaweza kuwekwa katika bahari tatu tofauti. Taja ukitolea sababu. (alama 3)
3. Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 4)
4. Huku ukidhibitisha, onyesha jinsi mshairi alivyotumia idhini yake ya kishairi. (alama 4)
5. Taja na uonyeshe mbinu za lugha zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)
6. Andika ubeti wa sita katika lugha tutumbi. (alama 4)
7. Eleza maana ya maneno haya kwa mujibu wa shairi. (alama 2)
 - a. Shina
 - b. Wima

FASIHI SIMULIZI

7

- (a) Jadili sifa za miviga. (Alama 5)
- (b) Fafanua sifa za ngomezi. (Alama 5)
- (c) Eleza umuhimu wa ushairi simulizi huku ukitoa mifano mwafaka. (Alama 5)
- (d) Jadili hatua za ukusanyaji wa data. (Alama 5)